




MUHTASARI WA MODULI YA MFUMO SHIRIKISHI WA UHAKIKI (PGS)

Umeandaliwa kwa kuzingatia mwongozo wa mafunzo ya Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) ulioandaliwa na TOAM kwa kushirikiana na wadau wa PGS Tanzania



MAANDALIZI YA MAARIFA HAYA

- Nakala hii ni tafsiri ya kiswahili ya mwongozo wa mafunzo ya Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) uliotengenezwa awali kwa lugha ya Kiingereza kupitia ushirikiano wa shirika la kilimohai Tanzania (TOAM) na IFOAM – Organics International.
- Mwongozo huo ulishirikisha wadau wa PGS nchini Tanzania kuchangia ujuzi na maarifa ya namna mfumo huu unapaswa kutekelezwa.
- Kupitia mradi wa kitovu cha maarifa Afrika Mashariki (KHEA), TOAM iliweza kutafsiri mwongozo wa mafunzo haya kwa lugha ya Kiswahili ili kurahisisha matumizi yake kwa wadau mbali mbali wa mnyororo wa thamani. iliunga mkono tafsiri ya mwongozo huu kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili, kama sehemu ya kuwezesha upatikanaji na usambazaji wa maarifa kuhusu PGS.

UTANGULIZI KUHUSU MAARIFA HAYA

- Mwongozo huu wa Mafunzo ya Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) ni sehemu ya mfululizo wa nyenzo za mafunzo unaojumuisha moduli tano, zilizolenga kuwajengea washiriki uelewa na uwezo wa kutumia Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) katika Kilimohai.
- Nakala hii imejikita katika moduli 3 inayoangazia hatua za uanzishaji na uendeshaji wa PGS ikiangazia mchakato mzima na miundo ya kiuongozi.
- Nakala nyingine za mafunzo kwa ajili ya moduli zinazofuata zinapatikana kama sehemu ya mfululizo huu, hivyo watumiaji wanashauriwa kuzitumia kwa pamoja ili kupata maudhui kamili ya mafunzo ya PGS.

MODULE YA TATU

Utekelezaji na Uendeshaji wa Mfumo wa PGS

Muhimu: Seti hii ya slides za mafunzo kwa moduli ya 1-5 inapaswa kutumika kwa kufuata mwongozo wa Mtaala wa Mafunzo ya PGS kwa Wawezeshaji (ToT), 2025

3.1 Hatua za kuanzisha na kutekeleza mfumo wa PGS

Hatua za Utekelezaji wa PGS

Yaliyomo:

- Lengo la kujifunza
- Muundo wa kikundi cha PGS
- Kamati za PGS na majukumu yake
- Zoezi la 1: Mjadala wa vikundi kuhusu usimamizi wa PGS
- Hatua 7 za utekelezaji wa PGS



Hatua za Utekelezaji wa PGS

Lengo la kujifunza



Kuwawezesha washiriki kuelewa muundo wa kikundi cha PGS, majukumu ya kamati mbalimbali na hatua za utekelezaji wa PGS ili waweze kusimamia na kuendeleza mfumo wa PGS kwa ufanisi

Muundo wa Kikundi cha PGS

- PGS hujengwa juu ya ushiriki wa wadau mbalimbali wakiwemo wakulima, walaji, na wadau wengine wanaohusika katika mnyororo wa thamani wa bidhaa za kilimohai.
- Ili kuhakikisha uwazi, uwajibikaji na ufanisi wa utekelezaji, vikundi vya PGS huunda kamati mbalimbali kulingana na mahitaji na uwezo wa kikundi.

Muhimu: Hakuna muundo mmoja unaofaa kwa vikundi vyote vya PGS. Idadi na aina ya kamati zinaweza kutofautiana kulingana na ukubwa wa kikundi na mahitaji yake. Hata hivyo, Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ni kamati muhimu katika mfumo wowote wa PGS.

Kamati za PGS na majukumu yake

1. Kamati ya Usimamizi

- Kuratibu shughuli zote za PGS.
- Kusimamia utekelezaji wa maamuzi ya kikundi.
- Kusimamia kumbukumbu za kikundi.
- Kuratibu mikutano ya wanachama.
- Kuwasiliana na wadau mbalimbali kwa niaba ya kikundi.
- Kufuatilia utekelezaji wa mipango ya kikundi.

Kamati za PGS na majukumu yake...

2. Kamati ya ukaguzi wa ndani

- Kupanga na kufanya ukaguzi wa ndani wa mashamba.
- Kutathmini uzingatiaji wa viwango vya kilimohai.
- Kutambua maeneo ya maboresho kwa wanachama.
- Kuandaa taarifa za ukaguzi.
- Kuwasilisha mapendekezo kwa Kamati ya Uthibitishaji.



Kamati za PGS na majukumu yake...

3. Kamati ya Uthibitishaji

- Kupokea na kupitia taarifa za ukaguzi wa ndani.
- Kufanya maamuzi kuhusu uthibitishaji wa wanachama.
- Kushauri hatua za marekebisho pale panapobainika kutokuzingatiwa kwa viwango.
- Kufuatilia utekelezaji wa hatua za marekebisho.



Kamati za PGS na majukumu yake...

4. Kamati ya Mafunzo na Kujenga Uwezo

- Kubaini mahitaji ya mafunzo kwa wanachama.
- Kuratibu mafunzo ya PGS na kilimohai.
- Kuwezesha kubadilishana uzoefu na kujifunza kati ya wanachama.



Kamati za PGS na majukumu yake...

5. Kamati ya Masoko

- Kutafuta fursa za masoko kwa wanachama.
- Kuratibu shughuli za uuzaji wa bidhaa.
- Kukusanya na kusambaza taarifa za masoko.
- Kukuza matumizi ya alama ya Kilimohai katika masoko.



Kamati za PGS na majukumu yake...

6. Kamati ya Uzalishaji

- Kufuatilia uzalishaji wa wanachama.
- Kuhamasisha uzingatiaji wa kanuni za kilimohai.
- Kuhimiza matumizi ya pembejeo zinazokubalika.
- Kuwawezesha wanachama kuboresha uzalishaji.


Zoezi la 1

Maswali ya Kujadili

1. Kikundi chenu kina kamati zipi kwa sasa?
2. Kamati zipi zinafanya kazi vizuri?
3. Kamati zipi zinahitajika zaidi katika mazingira yenu?
4. Ni changamoto zipi mnazokutana nazo katika usimamizi wa PGS?
5. Ni mikakati gani inaweza kusaidia kuimarisha utendaji wa kamati za PGS?

Muhimu: Muwezesheji achague maswali kulingana na uelewa wake wa watu anaowafundisha na matarajio ya mafunzo

Hatua za Utekelezaji wa PGS



Hatua za Utekelezaji wa PGS

Hatua ya Kwanza: Uchambuzi wa Hali Halisi

- Uchambuzi wa wadau wa PGS ili kubaini mahitaji, vivutio na uwezo wa wadau mbalimbali.
- Kuelewa sheria na kanuni za kitaifa zinazohusu kilimohai na PGS.
- Kufahamu mahitaji ya soko na utayari wa walaji kulipia bidhaa zilizoidhinishwa na PGS.
- Kubaini Changamoto za ufikiaji wa masoko kama miundombinu na nyingine zinazowakabili wakulima wadogo.
- Kutambua uelewa wa kanuni na mbinu za kilimohai, hususan kwa wazalishaji.



Hatua za Utekelezaji wa PGS...

Hatua ya Pili: Kuunda Dira ya Pamoja

- Kuhakikisha wadau wote wanaelewa kwa wazi manufaa ya PGS ili kushiriki na kujenga ari ya kujitolea.
- Kuanza kwa kuandaa dira ya pamoja inayozingatia mahitaji na ustawi wa jamii husika.
- Kuwaleta pamoja wadau muhimu ili kukubaliana juu ya manufaa ya pamoja kama vile: Upatikanaji wa masoko, ubora wa bidhaa, bei za haki, msaada wa kiufundi



Hatua za Utekelezaji wa PGS...

hatua ya Pili: Kuunda Dira ya Pamoja...

- Kuchapisha na kuweka wazi dira ya PGS mahali ambapo wanachama wote wanaweza kuirejea.
- Kuwashirikisha wadau tangu mwanzo, kufafanua majukumu yao na kuhamasisha uchangiaji wa rasilimali kwa ajili ya uendelevu na utawala wa kidemokrasia.
- Kukuza ujifunzaji endelevu kwa kujenga uaminifu, kuimarisha ujuzi na kuongeza uelewa wa PGS miongoni mwa walaji na wadau wengine.
- Kuwakutanisha wadau muhimu ili kufikia makubaliano kuhusu manufaa watakayopata kama vile upatikanaji wa soko, ubora wa bidhaa, bei ya haki, na msaada wa kiufundi.

Hatua za Utekelezaji wa PGS...

Hatua ya Tatu: Kukubaliana na Kuweka Kumbukumbu za Jinsi PGS itakavyofanya Kazi.

- **Viwango Vilivyokubaliwa: Kuchagua** na kukubaliana kutumia kiwango kinachotambulika cha uzalishaji wa kilimohai (mfano EAOPS).
- **Muhtasari wa Viwango:** Kuandaa muhtasari kueleza kwa kifupi kanuni muhimu ili kuwa na uelewa wa pamoja miongoni mwa wanachama.



Hatua za Utekelezaji wa PGS...

Hatua ya Tatu: Kukubaliana na Kuweka Kumbukumbu za Jinsi PGS itakavyofanya Kazi.

- **Mfumo wa Usimamizi:** Kubainisha majukumu na wajibu wa viongozi, kamati mbalimbali na taasisi zinazosaidia utekelezaji wa PGS.
- **Mwongozo wa Taratibu:** Kuweka taratibu za:
 - Uthibitishaji wa ndani
 - Ukaguzi wa uzingatiaji wa viwango
 - Ushughulikiaji wa malalamiko
 - Kusitisha au kuondoa uthibitishaji pale inapobidi
 - Taratibu za kupokea mwanachama mpya



Hatua za Utekelezaji wa PGS...

Hatua ya Tatu: Kukubaliana na Kuweka Kumbukumbu za Jinsi PGS itakavyofanya Kazi.

- **Mwongozo wa kushughulika na ukiukaji:** Kuandaa orodha ya makosa na hatua za kuchukua kwa kila aina ya ukiukwaji.
- **Ahadi ya PGS:** Ahadi za PGS zinaandaliwa na kusainiwa kwa uwazi ahadi ya PGS na wazalishaji wote wanaoshiriki.
- **Vyeti vya Uthibitishaji:** Kutoa vyeti kwa kikundi kulingana na mfumo uliokubaliwa. Kuweka wazi wajibu na hatua zinazochukuliwa endapo viwango havitazingatiwa.

Hatua za Utekelezaji wa PGS...

Hatua ya Tatu: Kukubaliana na Kuweka Kumbukumbu za Jinsi PGS itakavyofanya Kazi.

- **Daftari la Wanachama:** Kutunza orodha iliyosasishwa ya wazalishaji walioidhinishwa.
- Kuwasilisha taarifa husika kwa TOAM au mamlaka husika kwa ajili ya matumizi ya Alama ya Kilimohai.
- **Matumizi ya Nembo/alama:** Baada ya kuidhinishwa, wanachama wanaweza kutumia nembo ya PGS au Alama ya Kilimohai kwenye bidhaa zao.



Hatua za Utekelezaji wa PGS...

Hatua ya Nne: Kujenga Uelewa wa Viwango na Kutoa Ahadi ya Kuvizingatia

- Kuhakikisha wanachama wapya wanajitoa rasmi kuunga mkono utekelezaji wa PGS.
- Kuongeza uelewa kupitia mafunzo na mikutano inayohusu viwango vya kilimohai, kanuni za PGS, taratibu za utekelezaji na hatua zinazoweza kuchukuliwa kunapokuwa na ukiukwaji
- Kuwashirikisha wanachama katika kuandaa rasmi mkataba au ahadi ya kufuata kanuni za PGS.



Hatua za Utekelezaji wa PGS...

Hatua ya Nne: Kujenga Uelewa wa Viwango na Kutoa Ahadi ya Kuvizingatia...

- Kutunza orodha ya wakulima wote wanaoshiriki katika PGS; vikundi kadhaa vya eneo moja vinaweza kushirikiana chini ya mfumo mmoja wa PGS.
- Kuwajumuisha wanachama wasiokuwa wakulima pale inapohitajika, huku majukumu na wajibu wao ukibainishwa wazi.

Muhimu: Wanachama wanapofahamu viwango na kujitolea kuvifuata, hujenga msingi wa uwajibikaji, uaminifu na ufanisi wa mfumo wa PGS



Hatua za Utekelezaji wa PGS...

Hatua ya Tano: Kuainisha na kujaza taarifa za mashamba

- **Kukusanya taarifa za shamba:** Kukusanya taarifa muhimu kwa mpangilio kila shamba la mkulima.
- **Mpango wa usimamizi wa shamba:** Kutumia mipango iliyopo ya usimamizi wa mashamba, au kuwasaidia wakulima kuiandaa iwapo haipo.

Taarifa muhimu zinazopaswa kujumuishwa katika mpango:

- Taarifa binafsi za mkulima/mzalishaji.
- Ramani ya shamba inayoonesha mgawanyo wa maeneo ya shamba, matumizi ya ardhi, mipango ya maendeleo ya baadaye n.k.

Hatua za Utekelezaji wa PGS...

Hatua ya Tano: Kuainisha na kujaza taarifa za mashamba...

Mambo ya Kuzingatia Katika Uchoraji wa Ramani

- Mashamba yaliyotawanyika katika maeneo tofauti yanapaswa kuwa na ramani zake binafsi.
- Mashamba yaliyo karibu au maeneo ya uvunaji wa mazao ya porini yanaweza kutumia ramani ya pamoja.

Uandaaji na uhifadhi wa taarifa

- Mpango wa usimamizi wa shamba unaweza kujazwa na mkulima mwenyewe au kwa msaada wa mtaalamu.
- Hakikisha kila mkulima anakamilisha mpango huo kwa kutumia kiolezo cha PGS, akipata usaidizi kutoka kwa wenzake au mratibu

Hatua za Utekelezaji wa PGS...

Hatua ya Tano: Kuainisha na kujaza taarifa za mashamba...

Uandaaji na uhifadhi wa taarifa..

- Mipango yote ihifadhiwe pamoja katika kumbukumbu za kikundi cha PGS.
- Mipango lazima ipitiwe wakati wa tathmini za wanakikundi wenza na iakisi hali halisi ya eneo husika



Hatua za Utekelezaji wa PGS...

Hatua ya Tano: Kuainisha na kujaza taarifa za mashamba...

Madhumuni na Matumizi ya Mpango wa Usimamizi wa Shamba

- Inaelezea historia ya shamba na mbinu za usimamizi.
- Hutumika kama rejea wakati wa kufuatilia maendeleo na kuongoza tathmini za wanakikundi wenza
- Hutumika kama ahadi ya maandishi (au ya mdomo) ya kuzingatia masharti kutoka kwa mkulima
- Inapaswa kujumuisha Ahadi ya Mkulima iliyotiwa saini na kuwa sehemu ya kumbukumbu ya taarifa za mkulima

Hatua za Utekelezaji wa PGS...

Hatua ya Tano: Kuainisha na kujaza taarifa za mashamba...

Kumbuka

Vikundi vya PGS katika Afrika Mashariki vinaweza kutumia fomu zilizorahisishwa na kuidhinishwa na Kamati ya Pamoja ya Usimamizi (JMC), zikiwemo:

- Fomu ya Maombi ya PGS ambayo hujazwa na kila kikundi.
- Fomu ya Ukaguzi wa ndani wa PGS ambayo hujazwa na Kamati ya ukaguzi

Muhimu: Wanakikundi wanaweza andaa fomu inayoendana na mazingira yao kwa kuzingatia misingi ya kilimohai na viwango vyake.

Hatua za Utekelezaji wa PGS...

Hatua ya Sita: Ufuatiliaji na ukaguzi wa ndani

Nini maana ya Ukaguzi wa ndani kwenye PGS?

- Ni pale ambapo wanakikundi mwenzako; wakulima, walaji au wadau wengine wanapotembelea shamba ili kutathmini mbinu zinazotumika katika uzalishaji.
- Huhakikisha uzingatiaji wa viwango vya kilimohai vilivyokubaliwa kupitia uthibitishaji wa Pamoja
- Ni kipengele muhimu katika mfumo wa PGS kwa kuwa hujenga imani , uwajibikaji na uwazi.
- Kila shamba linapaswa kukaguliwa angalau mara moja kwa mwaka.

Hatua za Utekelezaji wa PGS...

Hatua ya Sita: Ufuatiliaji na ukaguzi wa ndani..

Jinsi Ukaguzi wa ndani unavyofanyika

- Huandaliwa na mwezeshaji/mratibu au kamati ya usimamizi ya PGS na kutekelezwa na kamati ya ukaguzi.
- Hufanyika kwa ratiba maalum na kurekodiwa kwa kutumia fomu, na ripoti zilizokubaliwa.
- Mkulima anayefanyiwa tathimini lazima awepo ili kutoa maelezo na kupokea mrejesho.
- Tathimini hii huchochea kujifunza, ushirikiano na maboresho katika shughuli za kilimohai.



Hatua za Utekelezaji wa PGS...

Hatua ya Sita: Ufuatiliaji na ukaguzi wa ndani..

Faida za ukaguzi wa ndani

- Kuimarisha ujuzi na maarifa kupitia kujifunza kwa pamoja.
- Kusaidia kutafakari uboreshaji endelevu wa mbinu za kilimohai.
- Kuwashirikisha walaji ili wajifunze namna bidhaa zao zinavyozalishwa na kuongeza imani yao.
- Kupanua mtazamo wa wakulima na walaji kuhusu uzalishaji wa kilimohai.



Hatua za Utekelezaji wa PGS...

Hatua ya Sita: Ufuatiliaji na ukaguzi wa ndani..

Jinsi ya kuhakikisha ukaguzi unakuwa na ufanisi

- Kutoa maelekezo ya wazi na mafunzo kabla ya ukaguzi.
- Washirikishe wakaguzi wenye uzoefu kwa ajili ya ushauri katika hatua za awali.
- Kutumia fomu ya ukaguzi inayolingana na viwango vya kilimohai ambavyo kikundi kinafuata.
- Epuka maamuzi ya kibinafsi kwa kutumia vigezo vilivyokubaliwa.
- Kila ukiukwaji wa viwango uhusishwe na kipengele husika cha kiwango ili kuimarisha uwajibikaji.

Hatua za Utekelezaji wa PGS...

Hatua ya Sita: Ufuatiliaji na ukaguzi wa ndani..

Matokeo ya Ukaguzi wa ndani

Ripoti ya ukaguzi wa ndani inapaswa kuainisha:

- Majibu na maelezo ya mkulima.
- Mambo yaliyobainika na ukiukwaji wa viwango.
- Hatua za marekebisho zinazopendekezwa.
- Mbinu au bunifu chanya zilizobainika.
- Mapendekezo ya uthibitishaji.



Kumbuka: Fomu za ukaguzi wa ndani zinaweza kufanyiwa maboresho au kusasishwa mara kwa mara kadri inavyohitajika.

Hatua za Utekelezaji wa PGS...

Hatua ya Sita: Ufuatiliaji na ukaguzi wa ndani..

Tathmini ya Pembejeo za Kibiashara

- Ikiwa kuna shaka kuhusu pembejeo inayotumika:
 - Piga picha ya lebo au kifungashio.
 - Rekodi jina la bidhaa, mtengenezaji na viambato vilivyotajwa.
 - Wasilisha taarifa kwa TOAM kwa uhakiki.
 - Ikiwa taarifa haziko wazi, usitumie bidhaa hiyo hadi ithibitishwe kuwa inakubalika katika kilimohai.



Kumbuka: Ukaguzi wa ndani ndiyo msingi wa mfumo wa PGS kwa kuwa hujenga uaminifu, uwazi na kujifunza kwa pamoja miongoni mwa wanachama.

Hatua za Utekelezaji wa PGS... ✓

Hatua ya Saba: Uthibitishaji wa wanachama

Uthibitishaji wa matokeo ya ukaguzi wa ndani

- Kuhakikisha kuwa matokeo ya ukaguzi wa ndani yamekamilika kwa usahihi kulingana na taratibu za PGS.

Nani anawajibika kufanya uthibitishaji?

- Kazi hii hufanywa na kamati ya usimamizi ya PGS.
- Mifumo ya uthibitishaji hutofautiana baina ya vikundi
- Kamati ya uthibitishaji inatoa maamuzi ya uthibitishaji
- Kamati ya ukaguzi wa ndani inatoa maamuzi ya uthibitishaji.
- Kiongozi aliyeteuliwa, n.k.



Hatua za Utekelezaji wa PGS... ✓

Hatua ya Saba: Uthibitishaji wa wanachama...



- Majukumu ya Kamati ya Uthibitishaji
- Kamati ya Uthibitishaji (ikiwa na uwakilishi wa makundi mbalimbali ya wanachama) inapaswa:
- Kupitia ukamilifu wa ripoti za ukaguzi wa ndani.
- Kutathmini uzito wa mapungufu au ukiukwaji uliobainika.
- Kupendekeza hatua za marekebisho pamoja na muda wa utekelezaji wake.
- Kuthibitisha uamuzi wa mwisho wa uthibitishaji.
- Baada ya hapo, vyeti hutolewa kwa wanachama au kikundi

Hatua za Utekelezaji wa PGS...


Hatua ya Saba: Uthibitishaji wa wanachama



Hatua za Mwisho

- Wanachama wote wanaozalisha wanapaswa kufanyiwa ukaguzi na kuidhinishwa.
- Wanachama walioidhinishwa wanapaswa kusaini ahadi ya pamoja ya PGS.
- Kikundi kuwasilisha ombi la kutumia alama ya kilimohai TOAM kwa ajili ya taratibu zingine za ufuatiliaji.

Mchakato wa PGS



Zoezi la 2

Kuhusu mahitaji muhimu ya utekelezaji wa PGS na nyaraka zinazohitajika



Muda: Dakika 30

HITIMISHO

- Moduli hii imeangazia hatua za kufuata katika kuanzisha na kutekeleza Mfumo shirikishi wa Uhakiki (PGS). Hatua hizi ni za muhimu ili kujenga PGS imara na yenye manufaa kwa wazalishaji na walaji wa bidhaa za kilimohai.
- Katika Moduli ya 4 utajifunza zaidi kuhusu uhusiano uliopo kati ya viwango vya kilimohai vya Afrika Mashariki vijulikanavyo kama East African Organic Products Standards (EAOPS) na mfumo wa PGS.

*Imeandaliwa na Shirika Mwamvuli la Kilimohai Tanzania
(TOAM) kupitia mradi wa kitovu cha maarifa Afrika Mashariki
(Knowledge Hub for Organic Agriculture and Agroecology
Tanzania - KHEA)*

Kupata moduli nyingine tembelea jukwaa la kidijitali la maarifa ya
kilimohai na kilimoikolojia katika tovuti: <https://khea-africa.org/>

Tunapatikana:

Mtaa wa Samora Avenue, Jengo la Kelvin House, gorofa ya Kwanza.
Kwa mawasiliano Zaidi tupigie kupitia +25574413499